KUTOKA UNYWAJI WA POMBE YA MBEGE HADI UNYWAJI WA SODA YA CHUPA

Uhusiano baina ya dini na desturi ya unywaji katika jamii ya Wameru waishio Mlima Meru Kaskazini mwa Tanzania

Dr. Catherine Baroin[1]

Kitabu hiki kimetafsiriwa kwa Kiswahili na Aggrey MEENA kutoka makala ya Kifaransa ya Dr. Catherine Baroin (CNRS,UMR 7041, Nanterre, Ufaransa): ''De la bière de banana au soda en bouteille. Religion et boisson chez les Rwa du Mont Meru en Tanzanie du Nord'' iliyochapishwa katika jarida la Journal des africanistes . 2001, tome 71 fascicule 2 .pp. 77-94.

[1] catherine.baroin@mae.u-paris10.fr

UTANGULIZI

Mabadiliko ya kutoka kwenye unywaji wa pombe ya kienyeji, inayoitwa 'mbege' inayoandaliwa kwa kutumia aina fulani ya ndizi pamoja na ulezi (mbege), hadi kwenye unywaji wa soda ya chupa na chai katika jamii ya Wameru (Varwa kwa Kimeru) waishio Kaskazini mwa Tanzania hayamaanishi kuwa ni mabadiliko ya unywaji peke yake. Ni mabadiliko makubwa ya kijamii pia yaliyotokea katika kipindi cha kama karne nzima katika jamii hii ambayo pombe hiyo ya mbege ilikuwa na nafasi ya kipekee katika kuwezesha kuwepo kwa mahusiano ya watu na kubadilishana mawazo baina ya wanajamii, lakini mabadiliko haya ya unywaji yameigeuza kabisa jamii ya Wameru kuwa jamii ya kisasa inayojikita pia katika uchumi wa masoko (market economy). Unywaji wa pombe ya mbege ambao ulikuwa unafanywa zaidi na watu wazima au wazee, ulipigwa vita sana na Kanisa la Kilutheri ambapo walipinga pia baadhi ya tamaduni za kijadi na kuhimiza kilimo cha kahawa. Kilimo hiki cha kahawa kilisababisha mitindo mipya ya maisha. Kwa sasa, ongezekeo kubwa la idadi ya watu katika eneo la Mlima Meru limesababisha upungufu mkubwa wa ardhi na hivyo kusababisha matatizo kadhaa ya kiuchumi na kijamii pia.

Katika jamii nyingi za Kiafrika, pombe zinazotengenezwa kwa kutumia ndizi au ulezi (mbege) huwa zina umuhimu mkubwa katika mahusiano ya kijamii. Huwa ni chanzo cha kuchangamana na kustarehe pamoja, na huwa pia kichecheo cha uzalishaji mali, na pia kama namna fulani ya kuwasiliana baina ya watu hai na waliokufa au mizimu. Mara nyingine desturi hizi za unywaji wa pombe ya kienyeji hufanana katika jamii nyingi za Kiafrika licha ya umbali baina ya upande mmoja na mwingine wa bara hili, na wakati mwingine hufanana hata baina ya bara moja na bara lingine licha ya tofauti za kitamaduni na kijiografia. Katika hali hiyo, wataalamu wa mahusiano ya watu (comparative anthropology kwa Kiingereza) katika tafiti zao juu ya jamii za wanywaji wa pombe za kienyeji au za asili wanatoa matokeo ya kuvutia sana juu ya unywaji huo. Katika makala ya kitabu hiki nitaleta mchango mdogo wa ufafanuzi wa tafiti hizo kwa kuzungumzia umuhimu wa pombe ya 'mbege' katika jamii ya Wameru pamoja na kuporomoka kwa unywaji huo kufuatia mabadiliko ya kijamii na kidini yaliyotokea katika kipindi cha kama karne moja iliyopita.

KABILA LA WAMERU (VARWA kwa KIMERU)

Varwa (kwa Kimeru) ambao hujulikana zaidi kwa jina la Wameru[2], huishi upande wa kusini mashariki mwa Mlima Meru (wenye urefu wa mita 4,585) na ulio mkabala na Mlima Kilimanjaro nchini Tanzania. Idadi yao kwa sasa inafikia watu 250,000 (kwa takwimu za mwaka 2012) na wanaishi katika mazingira ya asili ambayo ardhi yake ya volkano ina rutuba nyingi na hupata mvua za kutosha kwa mwaka. Kama ilivyo kwa majirani zao Waarusha wenye asili ya kutoka Mto Nile (Nilotic) ambao huishi upande wa magharibi wa Mlima Meru, na pia Wachaga wa Kilimanjaro, Wameru hujishughulisha na kilimo cha mazao mbalimbali hususani kilimo cha

[2] Wameru wa Mlima Meru Tanzania hawana uhusiano na Wameru wa Mlima Kenya nchini Kenya.

kahawa kwa ajili ya kipato, na ndizi kwa ajili ya chakula. Ili kujiongeza kipato, Wameru hufuga mifugo kadhaa wakiwemo ng'ombe wanaofugwa kwa mtindo wa ufugaji wa ndani na pia hulima mahindi na maharagwe hasa katika mashamba yaliyo upande wa kusini chini mwa Mlima. Kwa sasa makazi yao yamesongamana sana kwa ajili ya uhaba wa ardhi unaosababishwa na ongezeko la watu ambao sasa husababisha kutawanyika kwa watu kwenda maeneo ya mbali.

Historia ya Wameru siyo ya zamani sana. Walihamia Mlima Meru na kuendelea kujijenga kidogo kidogo tangu karne ya 17. Kabla ya hapo hakukuwa na wakazi maalumu katika Mlima Meru zaidi ya baadhi ya vikundi vidogo vidogo vya wawindaji wanyama na wakusanyaji wa matunda ambavyo kwa sasa havipo tena. Mlima Meru ulikuwa ni hifadhi kwa wahamiaji wa muda wenye asili tofauti tofauti wakiwemo Washambaa kutoka Milima ya Usambara, Wamaasai kutoka nyanda tambarare za jirani na Mlima huo, pamoja na Wachaga kutoka Kilimanjaro hususani kutoka Machame. Lugha ya Kimeru (Kirwa)[3] ambayo wanaongea Wameru sasa ni lugha ya Kibantu inayofanana kwa karibu na lugha ya Kichaga cha Machame. Utamaduni wa Wameru na Wamachame unashabihiana katika nyanja nyingi.

Hakuna maelezo ya kutosha kuhusu jamii ya Wameru kabla ya kipindi cha uko loni kwa kuwa, tofauti na Wachaga, Wameru hawakushiriki katika biashara ya msafara iliyokuwa ikihusisha bidhaa za pembe za ndovu na watumwa kuelekea pwani ya Bahari ya Hindi. Ukweli huo unafanya Wameru leo kuwa na taswira nzuri juu ya historia yao. Kwa mujibu wa Wameru ni kwamba wazee wao hasa zamani waliishi maisha yenye neema nyingi ambapo pombe hasa ya mbege na nyama vilipatikana kwa wingi. Ili kupata utajiri, mwanaume alioa wanawake wengi ambao waliweze kulima eneo kubwa zaidi na pia kujihakikishia uzao wa kutosha wa watoto wengi katika jamii.

Ni kawaida kuwa kadri mtu anavyozeeka ni kawaida kukumbuka na kutamani mambo ya nyuma ya ujana wake. Wachunguzi wa mwanzo kutoka Magharibi (Ulaya) katika kipindi cha mwisho wa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 wanathibitisha jambo hilo. Wanaume wa Kimeru walikuwa na muda mwingi bila kufanya kazi yoyote na hivyo waliutumia muda huo ama kwa kujipumzisha nyumbani au kunywa mbege ya 'mbege' nyingi[4] wakati wanawake wao wakifanya kazi mbalimbali nyumbani au mashambani. Sherehe kubwa zilizojumuisha kunywa pombe na kula nyama zilikuwa zikifanyika mara kwa mara, ambapo pia mwanaume tajiri aliweza kuchinja ng'ombe kadhaa kwa ajili ya furaha binafsi ya kula nyama tu na kunywa pombe ya mbege ili kuwafurahisha jamaa na rafiki zake.[5] Desturi ya kuoa wake zaidi ya mmoja ilikuwa umeenea sana kwa Wameru kabla ya kuja kwa Ukristo. Wanaume matajiri kabisa waliweza kuwa na zaidi ya wake hadi 10; hata kwa hivi sasa unaweza kukuta wanaume wenye umri

---

[3] Kimeru (Kirwa) ni lugha ya toni (tone language) lakini nukuzi iliyotumiwa hapa imerahisishwa. Toni zenyewe hazijanukuliwa. R kubwa inamaanisha r ya midomoni (labial) wakati sh inatamkwa kama katika lugha ya Kingereza.

[4] Kwa mujibu wa Mmisionari wa Kijerumani, mwaka 1903, "One practically never finds (the men) at work, but usually around lazily or sitting and drinking beer" (Spear 1995:28).

[5] Baltazar Kaaya, 1978.

mkubwa wakiwa bado na wake watatu au wanne jambo ambalo siyo la kushangaza katika jamii ya Wameru.

Kumbukumbu waliyonayo wazee juu ya maisha ya neema wakati wa kipindi cha ujana wao ni kubwa sana ambapo hali ya maisha kwao ilikuwa nema kuliko sasa ambapo hisia za hali ngumu ya maisha ndizo zinazowatawala. Wanaume wengi wenye familia wana wasiwasi wa kushindwa kuwapatia watoto wao angalau vipande vya shamba vya kutosha kuishi kwa kila mmoja, hasa watoto wao wa kiume. Badala yake wanajutia maisha yaliyopita ambapo ardhi ilikuwa kubwa kuliko vile ambavyo waliweza kuilima na kuimiliki japo ukweli ni kwamba hata kwa kipindi hicho cha neema maisha hayakuwa ya neema kwa kila mmoja au kwa kila nyanja ya maisha. Kulikuwepo pia na madhaifu mengi. Hali ya wasiwasi ilikuwa kubwa, wanawake na vijana walikuwa na hadhi duni sana na umri wa kuishi ulikuwa mfupi. Hata hivyo kufuatia kuanzishwa kwa kwa kipato cha fedha kitokanacho na zao la kahawa, hali ya maisha ilibadilika sana na hata umri wa kuishi uliongezeka. Kipindi hicho nidhamu ilikuwa ya hali ya juu tofauti na sasa ambapo baadhi ya watu wakorofi wameongezeka sana. Kwa sasa familia nyingi zinafaidika na bidhaa za kisasa kwa matumizi mbalimbali, hata hivyo mambo na mahitaji mapya yamezaliwa ambayo pia yamekuwa chanzo cha mikanganyiko ya aina mbalimbali katika jamii hii.

Kwa ujumla katika kipindi cha karne moja jamii ya Wameru imebadilika kwa kiasi kikubwa. Wameru wametoka katika desturi ya kukutana na kustarehe pamoja, kutoka kwenye neema ya uchumi ambapo utajiri ulikuwa ukifurahiwa kwa pamoja, japo kwa maamuzi ya wazee wa kiume ambao ndio walikuwa na mamlaka ya maamuzi, hadi kwenye maisha ya kibinafsi ambapo unywaji wa mbege unapoteza nafasi yake katika jamii hii jambo linalokwenda sanjari na kupungua kwa mamlaka ya wazee katika jamii.

Pombe yenyewe, kama tulivyosema mwanzoni, hutengenezwa kwa ndizi na kimea cha ulezi. Kwa Kimeru, pombe hiyo huitwa waRi, ama mara nyingine huitwa kabisa jina kamili, yaani waRi wa umbi, kumaanisha 'pombe ya mbege' ili kuitofautisha na aina nyingine za pombe kama ile ya asali ama kwa Kimeru waRi wa ukyi. Ndizi mbivu humenywa na kuachwa au kuchemshwa katika maji kwa muda mrefu kidogo hadi pale rangi yake itakapobadilika na kuwa kama nyekundu. Baada ya hapo mchanganyiko huo wa maji na ndizi humiminwa katika vyombo vikubwa na kuachwa wazi kwa siku tatu. Maji kidogo huongezwa na kuachwa kwa siku nyingine moja. Kisha mchanganyiko huo huchujwa. Kwa sasa gunia jepesi ndilo hutumika kuchujia tofauti na awali ambapo walikuwa wakitumia kichujo kilichotengenezwa na khanga au kilichotengenezwa na majani ya mti aina ya nRuka.[6]

Ulezi ambao hulimwa kwa ajili ya kupikia uji na pia kwa ajili ya kutengeneza pombe, hulowanishwa na kuwekwa kwenye kichanja cha majani ya mgomba na kufunikwa na majani ya mgomba na kuachwa kumea ndani ya siku chache. Kisha hufunuliwa na kuanikwa ili ukauke katika sehemu ya wazi kwa siku kadhaa. Baada ya hapo, ulezi huo husagwa na unga wake huwekwa katika chungu kikubwa ambapo hupikwa na majikama uji. Kisha juisi ile iliyotokana na

[6] Mti huu haujafahamika sana.

kuchemshwa kwa zile ndizi mbivu huwekwa katika uji huo wa mbege pamoja na maji kwa kipimo maalumu. Mchanganyiko huo ambao hutengenezwa usiku huachwa usiku kucha na kesho yake asubuhi pombe huwa tayari kwa kunywa.

Pombe hii ya mbege ambayo hapo awali ilikuwa muhimu sana kwa Wameru itatusaidia katika kufuatilia mabadiliko ya jamii hii ya Wameru. Katika sehemu ya kwanza ya Kitabu hiki tutaangalia hali ya jamii ya Wameru katika kipindi cha mwanzoni kabisa wakati wa ukoloni, kwa maana ya kipindi cha mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 huku tukitilia mkazo katika umuhimu wa pombe hii ya mbege katika nyanja za mahusiano ya kijamii, na katika ibada na matambiko ya kijadi. Kisha katika sehemu ya pili tutaonyesha namna mabadiliko ya matumizi ya vinywaji yalivyotokea kutokana na mabadiliko yaliyoletwa na maendeleo ya kisasa sanjari na Kanisa la Kilutheri na kuanzishwa kwa kilimo cha kahawa.

JAMII YA WAMERU MWANZONI MWA KARNE YA 20

Kwa karibu miaka 100 iliyopita jamii ya Wameru ilikuwa ina mfumo wa kiutawala uliotokana na mihimili miwili inayotegemeana. Mfumo wa rika lililoundwa na uzao wa umri fulani unaokaribiana ambao uliwaweka wanaume katika makundi tofauti kulingana na kipindi cha jando, mfumo ambao uliimrisha mshikamano baina ya wanaume wa rika moja kutoka familia tofauti sanjari na kuhakikisha kuwa kunakuwepo na utulivu na heshima hasa kwa wazee. Mfumo wa pili ni ule uliokuwa umegawanya jamii ya Wameru katika ngazi ya koo kufuata upande wa kiume (patrilineal clans) ambazo ndizo zilizoshughulikia masuala ya kifamilia, mifugo na ardhi. Vilevile Wameru walikuwa na kiongozi wao mkuu aitwaye ‘mangi’ ambaye kwa kawaida hutoka katika ukoo maarufu hasa ukoo wa Kaaya, wakati ambapo ukoo wa Mbise ulikuwa ukoo maarufu katika masuala ya kidini hususani katika kuandaa na kufanya matambiko kama yale ya kuomba mvua.

WASHILI

Washili ni viongozi wa kimila. Upana wa mamlaka ya washili kabla ya ukoloni hayakufahamika sana na wakati wa ukoloni hawakuwa na mamlaka makubwa sana (Spear 1997:27). Kwa ujumla jamii ya Wameru ilikuwa jumla ya washili 16, ambapo mwanzoni walikuwa washili 9 hadi mwishoni mwa karne ya 19, ndipo washili wengine 7 waliongezeka kuanzia kipindi hicho hadi wakati wa uhuru wa Tanganyika ambapo utawala wa washili ulifutwa na kuwa mfumo wa machifu wa jadi. Hata hivyo ukoloni uliwabadilisha washili hao na kuwa mawakala wa kisiasa ambao kazi yao kubwa ilikuwa ni kukusanya kodi ya serikali.

MFUMO WA RIKA

Mfumo rika katika jamii ya Wameru unafanana sana na ule wa jamii nyingine za Afrika Mashariki.[7] Makundi ya rika ama kwa Kimeru irika (umoja) na marika (wingi) ambayo yanahusisha kuwaweka katika kundi moja wanaume wenye umri unaokaribiana, yanatumika kuanzia enzi za asili ambapo idadi ya makundi hayo huongezeka kwa kadri muda unavyokweda. Mwanzoni mwa karne ya 20 idadi ya makundi haya ilikuwa 16 lakini sasa imeongezeka na kufikia 22.

Kundi la chini katika mfumo wa marika ni la vijana ama wasero kwa Kimeru (nsero kwa umoja) ambao hadhi yao inatofautiana kidogo na hadhi ya makundi ya wazee wao ambao hujulikana kama vasuri kwa Kimeru (nsuri kwa umoja). Kazi ya vasero ni kuhakikisha ulinzi kwa jamii, kazi ambayo huifanya chini ya uangalizi wa 'baba' zao waliopo katika kundi la pili juu yao yaani wazee. Wakati huo huo kundi jipya huundwa kwa kuhusisha vijana wa kiume wote waliofikia umri wa jando. Jando hufanyika kwa kijana mmoja mmoja au kwa makundi madogo madogo ambapo huusisha tohara ambayo hufuatiwa na kipindi cha mafunzo ya siri juu ya taratibu na desturi za kimila ikiwemo wajibu wa utunzaji wa wanawake na watoto. Vijana hao wapya huwa ni 'watoto' kwa wale waliopo kwenye kundi la juu yake baada ya lile la vasero kwa kuwa mara zote huwa na tofauti ya walau makundi mawili baina ya baba na mtoto wake.

Baada ya kipindi cha miaka 15 hadi 20, vasero hutoka katika rika la kuilinda jamii na badala yake watoto wao ndio nao hutakiwa kutahiriwa ili kujiandaa kuchukua rika la vijana. Hivyo kundi jipya hutakiwa kuundwa baina ya watoto na wazazi kwa kuwa watoto hawawezi kuwa katika kundi linalofuatana na lile la wazazi wao. Kwa kuwa vijana hao wote hutakiwa kutoka katika kundi moja tu kwa mara moja, kundi lililotangulia hufungwa kwa kupandishwa hadhi kwa kubadilisha kila kundi. Vasero hubadilika na kuwa'wazee' na hivyo kuwaachia vijana wapya majukumu yao ya awali.

Kubadilishana huko kwa marika na majukumu yao husindikizwa na sherehe kubwa ambapo rika la vasero wanaomaliza muda wao wa kuwa vasero huingia kwa heshima katika kundi la hadhi ya juu. Sherehe kubwa zinazohusisha pombe nyingi huandaliwa kwa gharama za wale wanaomaliza muda wao katika rika. Baadaye huandaliwa sherehe nyingine ambapo baba watachagua jina la kundi la rika jipya ambalo ni la watoto wao. Sherehe hiyo nayo huusisha unywaji mkubwa wa pombe za kienyeji hasa pombe ya mbege.

Mfumo huu wa rika haumaanishi tu kufanya karamu bali pia hupanga makundi ya wanaume katika ngazi mbalimbali zinazofuatana (kwa wasiopitia jando bado, kwa waliopitia jando, kwa vijana, na kwa wazee). Mfumo huu wa rika huwawezesha wazee kuwadhibiti vijana, huchochea mshikamano ndani ya kila kundi na kuhakikisha uwajibikaji na ulinzi thabiti kwa jamii nzima hususan kutokana na mpangilio wake imara wa marika hasa lile rika la vasero.

Pombe nayo inachukua nafasi muhimu sana katika mfumo huu. Siyo tu kwamba hunywewa kwa wingi wakati wa sherehe za rika bali pia ni alama ya hadhi

[7] Unafanana na ule wa jamii ya Meru Tigania-Igembe ya Kenya kulingana na utafiti wa A.M. Peatrik (1995-1999).

fulani hasa kwa kuwa ni wakubwa pekee yao ndiyo walioruhusiwa kunywa pombe. Usemi usemao: ‘niambie unachokunywa na mimi nikwambie wewe ni mtu wa aina gani’ ni usemi wenye maana kubwa katika jamii ya Wameru. Wakati ambapo rika la vasero lilikuwa na kazi kubwa ya kuhakikisha ulinzi pamoja na kufanya kazi nzito walizoelekezwa na wakubwa wao, bado hawakuruhusiwa kuburudika kwa kunywa pombe. Wakubwa wao walitumia muda wao mwingi kunywa pombe na kujadili masuala mbalimbali ya jamii yao.

Pombe pia ilikuwa ni namna ya kutuma ujumbe fulani. Kwa mfano, ili kutaka nao wapelekwe jando, watoto wa rika la vasero huwa hawasemi moja kwa moja, na badala yake huomba ‘ruhusa ya kutengeneza mbege’ ambapo huwaambia kwa siri watu wawili walioko kwenye kundi la wakubwa ambao ndio watakaowasemea. Wakubwa wanapokutana kunywa pombe hiyo ndipo huelezwa na wajumbe wale wawili. Hivyo pombe ilikuwa na nafasi ya lugha ya kificho kwa kusudi la kuwasilisha ujumbe au maombi fulani. Katika namna ya kipekee inaweza kutokea kwamba mzazi anataka mwanae wa kiume aingie katika kundi la juu kuliko lile alilotakiwa kuingia. Kwa hiyo mzazi huyo hutoa kiasi fulani cha pombe ya mbege na nyama kwa wale walio katika kundi analoomba ili watoe kibali kwa mwanaye. Hata hivyo pombe hiyo ya mbege na nyama siyo uhalali au kibali cha kukubaliwa kwa ombi lake bali maamuzi hutegemea rika linaloombwa linaonaje. Kwa njia hiyo pombe ya mbege ilikuwa na nafasi muhimu sana na matumizi makubwa katika jamii ya Wameru ikiwmo kwa wanaume kukutana na kunywa pamoja na kufanya mazungumzo au wakatiwa sherehe na mahusiano mbalimbali ya kijamii ikiwemo pia maisha ya koo mbalimbali.

MFUMO WA UKOO

Jamii ya Wameru ina koo zipatazo 15 ambazo hufuata upande wa mwanaume (patrilineal) na kila moja inajitegemea kwa kiasi kiutawala. Kila ukoo unaye kiongozi wake wa uko (nshili wa ufwaRi) na pia kila ukoo unajgawa tena kiutawala kulingana na ukubwa wa maeneo wanayoishi. Hata hivyo kila ukoo una eneo lake la asili ambalo kwa kawaida ndilo eneo lake la kufanyia sala, ibada na matambiko maalumu. Maeneo ya asili ya ukoo yalifuata historia na utamaduni wake unahusishwa na historia ya mzimu wa kale au mwanzishi wa ukoo husika.

Masuala yote yanayohusu maisha binafsi ya mtu hususan masuala ya ndoa pamoja na ardhi yalikuwa yanashughulikiwa ndani ya ukoo wa mtu husika. Kwa mfano, masuala ya migogoro ndani ya ndoa au familia, migogoro ya urithi, hatma ya mjane na yatima, na matatizo ya mipaka ya mashamba yalikuwa yanashughulikiwa kwanza na kiongozi wa familia ya upande wa baba akishirikiana na watoto wake wa kiume waliooa. Endapo suluhu haijapatikana, basi rufaa hufanyika kwa kuhusisha baadhi ya ndugu wengine, na endapo pia suluhu haikupatikana, basi kiongozi wa ukoo wa eneo husika hupokea suala hilo na kulishughulikia na ikibidi atahusisha ukoo wote.

Kikao chochote cha ukoo kilikuwa hakiwezi kufanyika bila ya kuwepo kwa pombe ya mbege. Mtu yeyote aliyekuwa anataka kuwasilisha suala lake ili lijadiliwe na kikao cha ukoo alitakiwa kutos kiasi fulani cha pombe ya mbege ambayo ilikuwa

ikinywewa na wana ukoo huku wakiendelea kujadili masuala husika kwa ajili ya kuyapatia ufumbuzi. Pombe ndiyo ilikuwa kichocheo muhimu katika kikao.

Ukoo haukuwa tu na mamlaka katika masuala ya kiutawala bali ulikuwa na hadi sasa bado unaendelea kuwa ni alama ya umoja na chanzo cha mshikamano miongoni mwa wana ukoo. Kosa la mauaji ndani ya ukoo lilikuwa ni jambo la ndani ya ukoo na halikuwa na fidia lakini endapo muathirika wa mauaji alikuwa ni mtu kutoka ukoo mwingine, basi wana ukoo wote walichangishana ili kulipa fidia ambayo ilikuwa ni ng'ombe 49 kulipwa kwa ukoo wa mtu aliyeuawa ili kuepuka kulipiziwa kisasi na ukoo huo wa mtu aliyeuawa. Utamaduni wa Wameru uliweka pia viwango vya fidia ya makosa kama kujeruhiwa na kupigwa ambapo viwango vya kiasi fulani cha pombe ya mbege vilivyotakiwa kutolewa kwa ajili na kiasi kilitofautiana kulingana na aina na ukubwa wa kosa. Kwa upande mwingine kama mtu atafanya kosa na kuficha au kosa kutoadhibiwa, basi yeye ama ndugu zake wa familia yake au hata ukoo mzima na hata mifugo yake wangekumbwa na majanga kama vile ugumba, magonjwa na hata vifo.

Kwa hiyo majanga yote yalikuwa yanatafsiriwa kwa mtazamo wa makosa fulani yasiyoadhibiwa wala kupatiwa suluhu na kwamba pale mtu anapopatwa na janga fulani lililo asili ya ukoo fulani, basi hiyo huwa moja ya alama kwamba mtu huyo ni mmoja wa wana ukoo husika. Koo zilizaliwa kama tokeo la kukua kwa familia na zilikuwa zikishiriki katika matukio yote makubwa ya kifamilia. Haya yalionekana katika matukio kama ya ndoa ambapo baada ya makubaliano baina ya familia mbili husika mpango wa ndoa ulikuwa ukihalalishwa kwa familia ya mwanaume kutoa kiasi fulani cha pombe ya mbege kwa ukoo anakotoka mwanamke anayetarajiwa kuolewa. Wana ukoo wote wa bibi harusi mtarajiwa hualikwa na kunywa pombe hiyo kwa kugawana ikiwa ni alama ya kukubali posa ya ndoa.[8] Unywaji huo wa pombe ya mbege katika makubaliano ya uchumba ulijenga mazingira ya kufahamiana kati ya pande mbili husika. Jambo hilo la kuja pamoja na kufahamiana na kujenga ukaribu na ushirikiano lilikuwa siyo tu jambo la kimila bali pia lilitawala maisha ya kidini ya Wameru hadi mwanzoni mwa karne ya 20.

MAISHA YA KIDINI NA KIMILA

Kabla ya Uristo, Wameru walifuata dini yao ya asili. Kimsingi dini ya Wameru ilikua na matmbiko mengi has ya kutambikia mizimu ya mababu. Mababu husika wailikuwa ni wale wazazi wa mwanzo wa wa familia, wa uzao mmoja, wa ukoo fulani ama wale wa jamii nzima ya Wameru kwa ujumla. Ili kupata baraka na mafanikio, mtu au ukoo au jamii nzima ilitakiwa kuijali na hata kuipa mizimu chakula mara kwa mara. Kwa upande mwingine, pindi patokeapo mambo mabaya au majanga kama vile ukame, ugumba, ajali, ugonjwa au mfululizo wa vifo tuhuma zilielekezwa kwa moja ya mizimu kuwa ndiyo chanzo na kwamba janga hilo ni matokeo ya mzimu kuchukizwa na kutopatiwa heshima ya kutosha. Hivyo ilitakiwa kufanyika tambiko maalumu na kuomba radhi kwa mzimu wenye hasira ili kumaliza tatizo. Kuna aina tatu za chakula cha tambiko kilichokuwa kikitolewa kwa mizimu:

[8] Utamaduni huo unafanana na ule wa jamii ya Dogon (Jolly 1995:439).

pombe (kwa mizimu ya kiume), maziwa (kwa mizimu ya kike) na wanyama waliotolewa hai au wakiwa wamechinjwa kama tambiko kwa ajili ya kumaliza tatizo au janga fulani katika familia, ukoo au jamii nzima.

Tambiko kubwa kuliko matambiko yote ambalo lilikuwa likifanyika karibu kila mwaka lilikuwani tambiko la kuomba mvua na ambalo kwa mara ya mwisho lilifanyika miaka ya 1984 na 1989. Kumbukumbu ya matambiko hayo bado ni kubwa sana miongoni mwa Wameru hadi leo. Kwa kawaida tambiko la kuomba mvua lilifanywa na jamii nzima na lilikuwa likifanywa kupitia watu wa ukoo wa Mbise kwa niaba ya Wameru wote. Utaratibu wake ulihusisha kwenda kwenye pango la mzimu wa kale alipoishi muasisi wa ukoo wa Mbise aliyeitwa Lamirei. Pango hilo lipo katika bonde la Mlima Meru upande wa mashariki. Watambikaji walipeleka chakula, pombe ya asali, maziwa kwa ajili ya mke wake na kondoo weusi wawili ambao waliachwa hapo pangoni baada ya kumuomba Lamirei awaletee mvua. Kwa sasa pombe hiyo ya asali ambayo ilikuwa ikitolewa kwa mizimu imebaki kuwa pombe inayopendwa zaidi na wazee japo kwa muda mrefu sasa pombe ya mbege imekuwa ikipata umaarufu zaidi katika matumizi ya kawaida na hata yale ya kiibada.

Kwa takribani karne moja iliyopita matambiko mengi ya kimila ya mtu mmoja mmoja au ya kikundi yamekuwa yakitumika kurekebisha masuala magumu ya maisha ya kila siku. Kila ukoo ulikuwa na sehemu yake maalumu ya kufanyia matambiko, iwe ni chini ya mti mkubwa au mlima au pango fulani penye asili ya historia yao ambapo ndipo wanapokuwa wanafanyia matambiko yao na kutoa kafara kwa mizimu yao mara kwa mara. Wakati wa matukio makubwa kama vile kuzaliwa kwa mtoto, kutolewa kwa jina ama msiba, kila kiongozi wa familia au ukoo alikuwa akiwapa heshima wakubwa zake has wale waliomtangulia. Mkuu wa familia au ukoo alikuwa na wajibu wa kidini pia, kwa mfano kuandaa na kuongoza matambiko kama yale yaliyohusisha maziwa au pombe katika eneo la familia husika ambalo mara nyingi huwa ni penye mwamba mkubwa au chini ya mti mkubwa. Mkuu huyo wa familia au ukoo alikuwa na wajibu wa kuhusisha mizimu na matukio mbalimbali katika eneo lake au kwa watu wake na hivyo kuomba baraka zao.

Mara chache damu au sehemu ya nyama ya mnyama fulani ilitolewa kama chakula anachopewa mzimu hususani katika tambiko linalohusu au linaloomba kuzaliwa kwa mtoto. Nyama inayobaki katika mnyama aliyetolewa sehemu yake kwa ajili ya tambiko huliwa na watu wa familia au ukoo husika. Maisha ya imani za kimila yalikuwa maingiliano makubwa sana na maisha ya familia au ukoo husika. Katika shughuli yoyote ya familia au ya ukoo inayohusisha vyakula au vinywaji pombe ya mbege ndiyo ilikuwa ikichukuwa nafasi ya kwanza na umuhimu zaidi, hivyo basi pombe ya mbege ilikuwa pia mhimili muhimu sana katika maisha ya imani au dini kwa jamii ya Wameru.

FAMILIA

Pombe haikuwa ikitumika tu kwa sababu za kiimani kama matambiko na mawasiliano na wafu au mizimu, bali pia ilikuwa ni njia ya kuimarisha mahusiano ya kijamii baina ya walio hai. Hata kabla matambiko watu walikutana na kuweka mipango ya matambiko ambapo pombe ya mbege ilinyweka kwa wingi. Mtindo huo

wa kuonyesha ushirikiano na mahusiano kwa njia ya kunywa pombe pamoja ulikuwa umetawala sana katika rika, ukoo na familia.

Familia nyingi zilihusianisha pombe na mambo yanayohusiana na uumbaji wa binadamu. Kwa mfano, ujauzito wa mwanamke ulikuwa ukifananishwa na utengenezaji wa pombe ya mbege, kama inavyosemwa katika usemi: "mbege iliyoiva sana haitoi pombe nzuri," kwa Kimeru: *mimia shiiya iiraa waRi ndi,* ikiwa na maana kuwa mwanamke mwenye umri mdogo hawezi kuzaa mtoto mzuri (Harjula 1997:101). Hivyo pombe nzuri inaonekana kama taswira ya mtoto mzuri na mwenye afya njema[9]. Hadi kufikia mwanzoni mwa karne ya 19 ilikuwa siyo kawaida kabisa kwa msichana wa Kimeru kupata mtoto kabla ya kuolewa. Uhusiano wa kuoana ulifuata mchakato mrefu, kuanzia posa hadi ndoa, mchakato ambao ulihusisha mfululizo wa utoaji wa mahari ambayo sehemu ya mahari hiyo ilikuwa utoaji wa pombe ya mbege. Ili mzazi wa kijana wa kiume aweze kuwasilisha ombi la kijana wake kuoa kwa mzazi wa binti, alitakiwa kupeleka pombe ya mbege kiasi cha nusu debe kwa mzazi wa binti siku ambayo anakwenda kuwasilisha ombi hilo. Kisha mara baada ya posa hiyo kukubaliwa, familia ya mwanaume anayetaka kuoa hutakiwa kutoa kwa familia ya mwanamke anayeolewa, pombe ya mbege au debe la asali ili kutengeneza pombe ya asali ambayo watakunywa ndugu wa ukoo wa mwanamke ili kuwaarifu juu ya mipango ya uchumba kwa binti wao. Wakishaelezwa na baba au ndugu wa karibu wa msichana, wana familia hao au wana ukoo huo hunywa pombe hiyo ya mbege kama ishara ya kukubali posa. Hata hivyo kama hawakubaliani na posa hiyo, bado pombe hiyo hunyweka na gharama zake kamwe hazirudishwi. Kwa upande wa ndugu wa mwanaume anayeoa nao pia huitwa na kuarifiwa na kisha hualalisha uchumba wa kijana wao kwa kutengeneza na kunywa pombe ya mbege.

Mifugo kadhaa pia huendelea kutolewa kama mahari kutoka kwa familia ya kijana anayetaka kuoa kwenda kwa familia ya binti anayeolewa na baada ya hapo baba wa binti na familia yake hupewa tena pombe ya kuwaomba kupanga pamoja tarehe ya harusi. Ili mipango yoyote ya kuoana ikubalike ilitakiwa lazima bwana harusi awe ametahiriwa na hata pia bibi harusi naye awe amefanyiwa tohara. Mara nyingi tohara kwa bibi harusi ilifanyika huku bwana harusi akiwepo kushuhudia na kisha kuwekwa ndani hadi atakapopona (Purrit 1970:81). Baada ya harusi bwana harusi aliweza kupewa chumba maalumu na mke wake kule kwa wakwe na kisha upande wa bwana harusi wangeandaa tena pombe ya mbege ili kijana aweze kumuomba baba mkwe wake ruhusa ya kumchukua mke wake na kumpeleka nyumbani kwake. Kwa ujumla desturi ya kuoana ilikuwa inahusisha mfululizo wa maandalizi na utoaji wa mahari vilivyoohusisha utoaji wa pombe ya mbege kwa kiwango kikubwa. Kila hatua ya mchakato wa harusi ilihusisha unywaji wa pombe wa mbege jambo linalofanya pombe hiyo kuwa na umuhimu mkubwa kawa Wameru.

---

[9] Katika jamii ya Dogon, ambao pia ni wanywaji wakubwa wa pombe kama Wameru na ambao pia pombe inachukua nafasi kubwa katika jamii, uhusiano unajengwa baina ya utengenezaji wa pombe na kuzaliwa kwa motto (Jolly 1995:490). Bila shaka kufanana huku kunakoonekana katika jamii hizi mbili za wanywaji wakubwa wa pombe na ambazo hazina uhusiano wa kiuzazi na wala ukaribu wa kijiografia, hakuna chochote cha kipekee.

Kama ilivyo hata sasa wanawake wanapoolewa waliziacha familia zao na kwenda kuishi kwa waume zao. Kwa kipindi cha nyuma, na hata sasa kwa sehemu fulani, kila kijana alipooa alipatiwa sehemu ya shamba na baba yake kwa ajili kulima kwa mahitaji yake ya chakula nyumbani. Ili baba atoe shamba hilo kijana wake alipaswa kuandaa kiasi fulani cha pombe ya mbege ili kumuomba baba yake na ndugu wengine wa karibu kumuonyesha shamba lake. Baba pia alimpatia mwali wake ng'ombe kwa ajili ya kutunza na kupata maziwa. Baba bado alikuwa na mamlaka juu ya watoto wake wa kiume hata baada ya kuoa na kwa kawaida walikuwa wakiendelea kuishi jirani. Mtoto wa mwisho wa kiume alikuwa na jukumu la kuwatunza wazazi wake pindi wanapozeeka na yeye ndiye alikuwa akipata sehemu kubwa ya urithi ikiwemo makazi ya baba yake. Hata hivyo wakati mwingine utaratibu huo wa kumhenzi zaidi mtoto wa mwisho wa kiume ambao unafanana na ule wa jamii ya Wachaga wa Kilimanjaro, ulikuwa ukiamsha hisia za wivu baina ya watoto wa kiume wa familia moja kama anavyoeleza Moore (1986) kuhusu Wachaga.

Endapo mtoto atakiuka maadili na kukataa komba radhi, basi mzazi aliweza kumwachia laana na athari za laana hiyo zilikuwa zikiogopwa sana. Hata hivyo laana hiyo iliweza kuondolewa kwa motto mhusika kuomba radhi kwa heshima kwa baba yake au kwa mtu wa rika la baba yake endapo baba yake atakuwa amefariki. Ili kupata msamaha huo mhusika alitakiwa kuchinja mbuzi dume na kutoa pombe ya mbege kwa baba yake na wanandugu wengine. Watu wa rika moja na baba walikuwa wakihusishwa na walishiriki kunywa pombe hiyo kama ishara ya kukubaliwa msamaha wake na kuondolewa laana, kwa kutangaziwa msamaha au pia wakati mwingine wazee walifanya ishara ya kuitemea mate pombe ambayo iliandaliwa kwa kunyweka kama ishara ya kutoa Baraka kwa mhusika.

Kama vile pombe ilivyokuwa muhimu katika hatua za kuondoa laana, ndivyo pia kinyume chake ilikuwa njia kubwa iliyotumiwa na wachawi (kwa Kimeru vasavi au nsavi kwa mmoja) kwa ajili ya kuloga watu. Kwa ajili ya hofu ya kudhurika kupitia unywaji wa pombe imekuwa ni kawaida kwa mtu anayempa mwenzake pombe kuionja kwanza kabla ya kumpa mtu mwingine ili kumaanisha kuwa pombe hiyo ni salama. Tendo hilo la kuria au kuonja kwanza pombe hujulikana kama 'kutoa mende, ama kwa Kimeru 'uta ngishe tafo.'[10] Kwa jinsi hiyo hiyo mke huonja chakula alichomuandalia mume wake mbele yake au anapompa mtu mwungine yeyote chakula, hasa chakula cha asili kiitwacho 'loshoro.' Desturi hii ya kuonja chakula bado inaendelea hata leo hasa kwa wanawake wazee.

Ndoa za wake wengi ni jambo lililokuwa likifanywa na wanaume wengikatika jamii ya Wameru kama njia ya kupata nguvu kazi na kwa vile ardhi ya kulima ilikuwa kubwa na ya kutosha. Kila mke alipaswa kulima shamba lake na kuendesha maisha yake na alikuwa pia na sehemu ya ardhi kwa ajili ya mifugo japo umiliki wa mali zote ulikuwa mikononi mwa mwanaume.

UCHUMI

Uchumi wa Wameru ambao kwa sehemu kubwa ulitegemea kilimo na ufugaji ulikuwa unachochewa sana na hali nzuri ya hewa. Ardhi yao yenye rutuba nyingi

[10] Sikuweza kupata sababu ya kutumika kwa neno mende katika usemi huo.

inatokana na udongo wa kivolkano wa Mlima Meru na hupata misimu miwili ya mvua kwa mwaka huku umwagiliaji wa kila siku ukifanyika kwa baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwaka kilichobaki. Maji hayo ya umwagiliaji yanatokana na mifereji inayotoka mlimani. Rutuba ya ardhi inachangiwa pia na uwekaji wa mara kwa mara wa samadi inayotokana na ufugaji wa ng'ombe na wanyama wengine wadogo wadogo. Ndizi ambazo kilimo chake huwa hakihitaji gharama nyingi na mavuno yake hupatikana kwa kipindi chote cha mwaka husaidia kuhakikisha upatikanaji wa hakika wa wa chakula. Ng'ombe na mifugo mingine walikuwa vilihudumiwa na mama na watoto wake kwa kuletewa chakula na wakati mwingine walichungwa na watoto katika eneo filani la pamoja. Mifugo ilikuwa ikitumika kwa chakula na pia katika utoaji wa mahari wakati wa kuoa na pia katika uandaaji wa tafrija kubwa za kula nyama. Ndizi na mahindi ndivyo vyakula vikuu vikiliwa na nyama au maharagwe pamoja na mboga mboga nyingine.

Pombe ya mbege ilikuwa ni kinywaji muhimu kijamii na ilitengenezwa kwa wingi kila siku kwa kuuza au kubadilisha na bidhaa fulani na hivyo ikawa pia nguzo ya kiuchumi. Kama tulivyoona pombe ya mbege ilikuwa na nafasi ya kipekee katika kila sekta ya maisha kuanzia kuzaliwa hadi kufa na hata baada ya kifo kwa kuwa hata wafu pia walipewa sehemu yao ya pombe. Pombe ilikuwepo katika vikao vyote muhimu vya wanaume. Ilikuwa pia ni alama ya kutofautisha hadhiya makundi baina ya vijana (*vasero*) na wale wenye umri wa makamo (*vasuri*). Vasuri walitumia muda wao mwingi kunywa pombe.[11] Kwa kifupi pombe ilikuwa ikitengenenezwa na kunywewa kwa wingi katika jamii iliyokuwa na wingi wa neema na ambapo majukumu yalikuwa yameanishwa vyema: kwa wanawake waliotakiwa kuhakikisha uzalishaji wa chakula; vijana walijihusisha na ulinzi wa jamii; na wanaume wenye umri wa makamo waliweza kuwa na muda mwingi bila kazi kubwa na hivyo kukutana pamoja na kunywa pombe kwa kadiri watakavyo na kujadili mambo mbalimbali ya jamii yao. Hata hivyo wakati mwingine kulikuwa na hali ya hofu hasa ya hali ya hewa, kama mwishoni mwa karne ya 19 kulitokea mfululizo wa majanga ya hali ya hewa ambayo yaliutangulia kidogo ujio wa ukoloni ambao nao pia ulisababisha mabadiliko makubwa katika jamii ya Wameru.

KARNE YA MABADILIKO YA KIJAMII

Hapa nitazungumzia kwa kifupi tu kuhusu mambo ambayo kwa kipindi cha karne moja yamesababisha badiliko moja baada ya jingine katika nyanja zote za maisha ya Wameru. Umuhimu wa pombe kijamii ambao umeelezewa kwa kina katika sehemu iliyopita unabaki kuwa ndiyo msingi wa maelezo hayo kwa kuwa namna ya unywaji wa pombe imekuwa ikibadilika taratibu jambo ambalo linathibitisha uwepo wa mabadiliko katika Nyanja nyingine za maisha ndani ya jamii hii.

Mchangamano wa kwanza baina ya Wameru na Wazungu mwishoni mwa karne ya 19 ulienda sambamba na mfululizo wa majanga (kama vile ya magonjwa ya ng'ombe hasa ndui, uvamizi wa nzige, na ukame), yaliyoikumba Afrika Mashariki kwa ujumla.[12] Licha ukweli kwamba kwa wakati huo Wameru

[11] Angalia Spear (1995:28); Puritt (1970:103).
[12] Angalia Iliffe 1979:124.

hawakuwa wameanza kujihusisha sana na biashara, bado waliathiriwa pia na majanga hayo na bila shaka hali ya wasiwasi iliyotokana na majanga hayo ndiyo iliyopelekea jaribio la kwanza la Wazungu kuingia katika jamii ya Wameru mnamo mwaka 1896, jaribio ambalo liligeuka kuwa jambo la kusikitisha. Habari ya kusikitisha ya jaribio hilo inahusu Wamisionari wawili kutoka Kijerumani ambao licha ya kuwa na ridhaa ya Nshili, waliuawa na vijana wa Kimeru kwa ushirikiano na vijana wa Kimaasai. Tukio hilo la mauaji liliwafanya Wakoloni kuiona jamii ya Wameru kama jamii pinzani dhidi ya Ukoloni.

Mashambulizi yaliyofanywa dhidi ya Wameru na wakoloni Wajerumani, ambao walikuwa wamejizatiti katika Mji wa Arusha muda si mrefu, yalikuwa ya kutisha. Sehemu kubwa ya eneo la Meru likaharibiwa sana na mashambulio hayo. Nshili wa Wameru akanyongwa, warithi wake wawili wakafungwa gerezani na mfumo wa utawala wa jadi ukabadilishwa mara moja na kuwa chombo cha kutekeleza sera za wakoloni.

Hata hivyo kuuawa kwa Wamisionari hao wawili mwaka 1896 hakikukatisha tama chama cha Wamisionari wa Leipzig ambapo mwaka 1902 walirudi tena na kuingia katika jamii ya Wameru chini ya ulinzi wa Wajerumani na baada ya miongo kadhaa Kanisa la Kilutheri likawa ndilo Kanisa pekee la Kikristo katika jamii ya Wameru. Licha ya ari kubwa waliyokuwa nayo wachungaji wa Kilutheri bado Ukristo ulipata mapokezi ya polepole hasa kutokana na msimamo wa Kanisa la Kilutheri ulipingana kwa kiasi kikubwa na baadhi ya tamaduni za Wameru. Hivyo haikuwa tu kwamba Wachungaji walikuwa na kazi ya kueneza dini hii mpya ya Kikristo bali pia walikuwa na kazi kubwa ya kuanzisha maadili yao mapya na kupinga baadhi ya maadili ya kimila ambayo wao waliyaona hayafai, kama unywaji pombe na kutokufanya kazi kwa wazee, ndoa za wake wengi, ushirikina na uchezaji ngoma zinazoshirikisha mapenzi baina ya vasero na mabinti.

Katika juhudi za kuimarisha ushawishi wao kwa waumini wa mwanzo kabisa, Wamisionari walianzisha hosteli ambapo vijana walioingia Ukristo walipatiwa hifadhi na chakula na hivyo kuwa mbali na jamii nyingine ya Wameru.[13] Wakiwa kwenye hosteli hizo, vijana hao siyo tu kwamba walipokea mafundisho ya dini bali pia walifundishwa kuandika, kusoma na kuhesabu na kisha walikuwa wakifanya kazi katika mashamba ya kahawa ambapo mauzo ya kahawa hiyo yalisaidia kugharamia kazi za misioni. Kwa namna hiyo Kanisa halikuweka mkazo wake katika masuala ya kidini tu bali pia lilikuwa kinara mwanzilishi wa mambo mengine hasa mawili ambayo ndiyo vigezo vya mageuzi makubwa kwa Wameru. Mambo hayo mawili ni elimu na kilimo cha kahawa.

Amani iliyokuwepo baadye katika jamii ya Wameru chini ya utawala wa Wajerumani na kisha Waingereza iliwawezesha Wameru kurejesha kwa haraka maisha yao ya neema ambayo sasa yalipata kasi mpya kutokana na kukua kwa kilimo cha kahawa. Katika sehemu nyingi za wakulima wa Kimeru, kilimo cha kahawa kilianzishwa na mawakala wa Wamisionari. Wanafunzi wa Ukristo, wakiwa tayari wameelimishwa juu ya zao hilo la kahawa, waliuchukua mimea ya kahawa na kuipeleka majumbani mwao kwa kusudi la kuiotesha. Wakulima hao wa Kimeru walianza kuotesha kahawa kwenye mashamba yao ya migomba licha ya kitendo

---

[13] Angalia Spear (1995).

hicho kupata changamoto toka kwa wakulima wakubwa wa Kizungu waliokuwa na mashamba makubwa ya kahawa eneo la chini ya Mlima Meru ambao walitamani kuendeleza ukiritimba wao katika kilimo hicho chenye faida kubwa.

Idadi ya watu katika jamii ya Wameru iliongezeka kwa ustawi huo mpya na suala la upungufu wa ardhi likaanza kuwa tatizo kubwa. Kimsingi kwa muda sio mrefu sana maeneo yote ya kuzunguka Mlima Meru yalikuwa tayari yameoteshwa kahawa na kwa upande wa kusini kulikuwa na mashamba makubwa ya Wazungu yaliyozunguka karibu eneo zima la Wameru na hivyo kupunguza uwezekano kwa Wameru kupanua maeneo yao ya kulima na huku mashamba hayo ya Wazungu yakiwa yamezuia njia nyingi za kuelekea kwenye mifereji ya maji iliyotumika kunyweshea mifugo. Ili kutatua tatizo la uhaba wa ardhi, aliitwa mtaalamu Jaji Wilson ambaye aliwasilisha ripoti yake mwaka 1947. Katika ripoti yake hiyo, Jaji Wilson alipendekeza kuwa sehemu ya eneo la malisho lilipo upande wa Mashariki mwa Mlima Meru itengwe kuwa ukanda mpya wa mashamba ya Wakoloni.

Mpango huo wa Wazungu kuchukua eneo jingine la ardhi ya Wameru uliamsha upinzani mkali kutoka kwa Wameru. Hata Wakristo wa kwanza Wameru waliupinga mpango huo siyo tu kwa kuwa nao walikuwa wakulima wa kahawa bali kwa kuwa walikuwa wasomi waliojua kusoma na kuandika, hivyo walitafuta mwanasheria na kufungua mashitaka kwa Waingereza ambao ndio waliokuwa wakiiongoza Tanganyika chini ya uangalizi wa Umoja wa Mataifa (UN). Hivyo kukazuka kipindi cha mapambano dhidi ya Ukoloni. Kipindi hicho cha mapambano dhidi ya ukoloni ambacho kilijulikana kama Meru Land Case, pia kilichochea vuguvugu la kudai uhuru wa Tanganyika kitendo ambacho kimeendelea kuwa jambo la kujivunia sana kwa Wameru hata leo. Hii ilikuwa pia ni fursa kwa Kanisa la Kilutheri kuongeza ushawishi wake kwa Wameru kwa kuunga mkono harakati hizo na pia kuongeza mageuzi kadhaa ya kijamii ambayo tayari yalikuwa yamekwishaanza ndani ya jamii.

Hivyo kwa kupitia waumini wake wa kwanza ambao waliupinga mpango wa kuchukua ardhi zaidi ya Wameru sanjari na kuwapinga wakulima masetla wa Kizingu,[14] Kanisa la Kilutheru likawa limechochea mabadiliko mapya ya mafanikio kwa jamii. Kutokana na mafanikio yao kielimu, kisiasa, kimaadili na kiuchumi, Wakristo wa kwanza Wameru waligeuka kuwa kundi la wasomi wenye ushawishi na kuwa ndiyo mfano wa kuigwa na kufuatwa kwa asilimia kubwa na Wameru wengine. Dini ya Kikiristo ikazidi kupata waumini wengi pamoja na neema ya maisha iliyoletwa na fedha za mauzo ya zao la kahawa iliyowawezesha Wameru wengi kununua bidhaa mpya za kisasa pamoja na vyakula vilizotokana na uchumi wa masoko (market economy).

Ni wazi kuwa hali hiyo bora ya maisha ilisababisha mabadiliko makubwa katika misingi ya kimamlaka katika jamii ya Wameru. Kuanzia kipindi hiki, busara na mamlaka havikuwa tena mokononi mwa wazee peke yao bali sasa hata wanaume vijana wasomi na Wakristo walinufaika neema ya kusikilizwa katika jamii.

[14] Angalia Baroin 1998:542-543.

KANISA NA UNYWAJI WA POMBE

Bila kuchoka Kanisa la Kilutheri liliendelea kupinga ufahari wa wazee kwa kigezo cha maadili hususan kutokana na tabia yao ya unywaji mkubwa wa pombe. Kanisa hili halikukubaliana na tabia hiyo na hivyo likiwa linapinga vikali matumizi ya vilevi. Hivyo suala la unywaji wa pombe ambalo siku zote lilikuwa ni jambo la kifahari hasa kwa wanaume wenye umri wa makamo sasa likawa likipingwa vikali na Kanisa na kuelezwa kuwa ni maadili mabaya. Kwa kufanya hivyo Kanisa likawa limewapa vijana sababu ya kuhoji uhalali wa heshima kubwa ya kimaadili na mamlaka waliyokuwa wakipewa wazee, jambo ambalo lisingewezekana kabisa kipindi cha nyuma.

Unywaji wa pombe siyo tu kwamba ulipingwa na Kanisa bali pia ulikoma kuwa ni kitu cha wazee peke yao. Baadhi ya vijana walionufaika na hali nzuri ya kifedha iliyosababishwa na mfumo mpya wa uchumi, walitumia fursa ya mabadiliko hayo kujinunulia na kunywa pombe na hivyo kwenda kinyume na maadili ya Kikristo na hata yale zamani katika jamii yao. Wakati mwingine vijana wakishalewa waliwatukana hata wakubwa zao jambo ambalo linaweza kutafsiriwa kama ni kuwatukana mara mbili. Sifa ya kunywa pombe ilibadilika kutoka kuwa ufaharina kuwa uovu na kukoma kuwa jambo linalohusianishwa na umri wa mtu.

MAMLAKA YA WAZEE

Katika mapambano yake ya kiroho Kanisa lilipinga vikali mambo yote ya matambiko katika jamii ya Wameru. Kabla ya kuja kwa Ukristo, Wameru walikuwa tayari wakimwamini Mungu aliyeelezewa kuwa ni muumba wa dunia aitwaye kwa Kimeru *Iruva,* lakini kwa mujibu wao ni kwamba Mungu huyu hakuwa na ushawishi mkubwa katika jamii yao kuzidi mizimu yao. Ndiyo maana Baraka kutoka kwa wazee na ndugu wa karibu sana ndizo zilikuwa zinaaminika zaidi kuwa chanzo cha kufanikiwa na hali kadhalika laana zao ziliogopwa sana. Hivyo Wameru waliheshimu na hata kuwaogopa zaidi mababu zao kuliko hata *Iruva*. Kwa upande mwingine Kanisa lilifundisha kuwa ni Mungu (wa dini ya Kikristo) pekee ndiye mwenye uwezo wa kweli wa kuamua hatma ya kila mtu na kwamba hofu ya laana ni ya kipagani kwa kuwa ni sawa kuhoji uwezo wa Mungu. Kwa mujibu wa mafundisho ya Kanisa la Kilutheri ni kwamba muumini mzuri ni Yule anayeweka maisha na hatma yake katika mikono ya Mungu peke yake kwani ni yeye tu ndiye hulinda maisha na imani ya mtu dhidi ya hatari ya laana na ushirikina.

Kwa wazee wa Kimeru nguvu ya kuacha laana ilikuwa ni sifa muhimu kuanzia ngazi ya familia hadi kwenye ngazi ya juu ya mfumo ambao unafuata utaratibu wa makundi ya umri wa kuzaliwa. Kuikosoa nguvu hii kwa sababu ya mafundisho ya Kanisa kulizidi kuangamiza mamlaka ya wazee juu ya vijana. Kanisa lilitaka mamlaka ya wazee juu ya vijana yawe ni kwa upande wa kimaadili tu. Kanisa halikutaka tu kuchukua mamlaka na ushawishi waliokuwa nao wazee bali walitaka pia kupambana na adui mwingine ndani ya mfumo rika. Kwamba Wameru wa kwanza kujiunga na Ukristo walijikuta wakiachiwa laana na baba zao katika rika (jambo ambalo katika utamaduni wa Wameru ni sawa na kutishiwa kifo). Kadhalika walijikuta wakitengwa na wenzao wa rika moja. Kutengwa huko na wenzao

wa rika lao lilikuwa ni jambo la kuhofiwa sana kwani mshikamano baina ya watu wa kundi la rika moja ulikuwa ni msingi mkubwa sana wa kijamii kwa Wameru. Katika kuhimiza suala la maadili mema ya Kikristo, Kanisa la Kilutheri lilizidi kupinga sherehe zilizotokana na mfumo wa rika kama vile unywaji wa pombe katika sherehe za kusimikwa kwa makundi mapya ya rika zilisheheni uchezaji ngoma hasa usiku zilizochochea uasherati baina ya vasero na wapenzi wao.[15]

NDOA ZA WAKE WENGI

Ndoa za wake wengi ni suala lingine la kijamii kwa Wameru lilipingwa na Kanisa la Kilutheri lilofundisha kuwa ni kinyume kabisa na ndoa inayoaminiwa katika Ukristo. Hoja ya Kanisa kuhusu ndoa ya wake wengi ilionekana kuwajali zaidi wanawake na hivyo kufanya wanawake wengi kuingia katika Ukristo: waliona kuwa dini hiyo mpya ya Kikristo inawapa hadhi yao ya kimaadili na kijamii. Hata hivyo Wakristo wa kwanza walikumbana na nyakati nyingi ngumu: siyo tu kutengana na mshikamano wa makundi ya rika ya kimila bali pia kujitenga na ndoa za wake wengi kwa sababu kitendo cha kuwa na wake wengi kingewaondoa katika Kanisa. Katika suala la idadi ya watu, pengine kufifia kwa ndoa za wake wengi kulichangia kupungua kwa idadi ya watu kwa kiasi fulani pale mwanzoni japo baadaye idadi ya watu ilikuwa inaongezeka kwa kasi badala ya kupungua.

Kimsingi katika jamii ya Wameru, kabla ya ukoloni, mume alitakiwa kuepuka kujamiiana na mke wake kila baada ya mke kujifungua kwa muda wa miaka miwili au hata mitatu ambapo motto angekuwa ameacha kunyonya na kwamba katika kipindi hicho chote mume aliweza kufanya tendo la ndoa na wake zake wengine. Kuachwa kwa utamaduni wa ndoa za wake wengi kukawa ni mwisho wa utaratibu huo na hivyo desturi ya wanaume kujiepusha na tendo la ndoa mapema baada ya mke kujifungua ukawa nao umepungua kwa kiasi kikubwa sana.

Wakati huo huo mafundisho ya Kanisala Kiluteri kuhusu familia yalikuwa ni kama vile yanahimiza familia za Kikristo kuzaa watoto wengi bila ya watoto hao kupishana muda mrefu. Bila shaka mitindo hiyo mipya ya maisha sanjari na kuimarika kwa hali ya uchumi wa watu wengi kulichangia kuongezeka kwa idadi ya watu katiak jamii ya Wameru,[16] jambo ambalo lilisababisha kuibuka kwa tatizo uhaba wa ardhi ambalo linaendelea kuitatiza jamii hii hadi sasa hivi.

TABIA ZA ULAJI WA VYAKULA

Kuongezeka kwa idadi ya watu katika Mlima Meru kulileta athari nyingi na za moja kwa moja katika kilimo na pia ufugaji, athari ambazo zilisababisha pia

[15]Jamii ya Wameru hata hivyo haikuwa jamii yenye uhuru wa mahusiano ya mapenzi tofauti na ilivyo katika utamaduni wa jamii jirani ya Wamaasai.

[16]

Idadi ya Wameru iliongezeka kutoka watu 11,666 mwaka 1921 hadi watu 76,375 mw aka wa 1967 kwa mujibu wa Spear (1997:128).

kubadilika kwa tabia za ulaji vyakula. Maeneo ya pamoja ya kuchungia mifugo yalianza kupotea taratibu ili kupisha kilimo na hivyo ufugaji wa ndani ulianza kuchukua nafasi.[17] Baada ya Uhuru, jamii ya ng'ombe wa asili ilianza kuchanganywa na jamii ya ngo'mbe wa kisasa ama kuachwa kabisa bila kuzalishwa na wafugaji wakapendelea ng'ombe wa kisasa ha wale wa jamii ya 'friesian' ambao walihitaji chakula kingi zaidi japo pia walikuwa wakitoa maziwa mengi zaidi. Lengo halikuwa tena kuwa na idadi kubwa ya ng'ombe ili kuwatumia kwa ajili ya karamu za kula nyama na utoaji wa mahari bali lengo likawa ni kuwa na idadi ndogo ya ng'ombe wazuri wa maziwa kwa mtazamo wa kibiashara.

Matokeo ya mabadiliko haya yalisaidia sana kukidhi soko la mahitaji ya maziwa katika mji wa jirani wa Arusha ambayo yamekuwa yakiongezeka kutokana na idadi yake ya watu kuongezeka kila siku. Kuongezeka kwa mahitaji hayo kumekuwa kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko hata kipindi cha utawala wa Waingereza ambapo kwa sasa chai ya maziwa yenye sukari imekuwa ni kitu kinachopendwa karibu Tanzania nzima. Chai ya maziwa ni kinywaji kinachonywewa zaidi katika familia na ambacho pia ni kinywaji wanachopatiwa wageni wanapotembelea familia fulani. Hivyo Wameru waligeuka kuwa wazalishaji wa maziwa kwa ajili ya kuhudumia mahitaji ya mjini. Kwa sasa Wameru pia wamekua wanywaji wa chai ya maziwa kama Watanzania wengine licha ya kwamba wao hawalimi chai, kitu cha ajabu ni kwamba licha ya kuwa Wameru wanalima sana kahawa, wao siyo wanywaji wakubwa wa kahawa isipokuwa kwa nadra sana. Hapa ukweli unabaki kuwa huo ni mfano mwingine wa kubadilika kwa tabia ya vyajula katika jamii hii.

Kwa kiwango kikubwa Kanisa nalo linaunga mkono unywaji wa chai kwa kuwa ni kinywaji kisicho na kilevi. Hata watumishi wa Kanisa wanapokutana, kinywaji kinachotumika huwa ni chai. Kutokana na ushawishi wa Kanisa, unywaji wa pombe ya mbege katika mikutano ya kifamilia au jumuiya umepungua umaarufu wake maradufu. Katika sherehe za harusi, nafasi ya pombe ya asili ya mbege imechukuliwa na unywaji wa soda za chupa zinazozalishwa na kampuni tanzu za makampuni ya Kimarekani hasa soda za Coke Cola. Aina nyingine ya soda zinazonywewa zaidi ni pamoja za aina pepsi au mirinda kutoka kampuni ya Pepsi Cola. Ni soda hizo hizo pia ambazo hutolewa katika matukio kama ya utoaji wa mahari badala ya pombe kama ilivyokuwa ikitolewa hapo awali. Katika mikutano ya kidini, ambayo ni mingi sana siku hizi, vinywaji vinavyotumiwa ni soda au chai peke yake. Hali iko hivyo pia hata katika sherehe za kitamaduni za makundi ya rika,[18] ambazo kwa kawaida zilikuwa ni fursa ya kunywa pombe nyingi; na hivi sasa ni kwamba mara nyingine sherehe hizo zimekuwa zikiandaliwa katika mazingira ambayo wahudhuriaji wengi ni Wakristo hasa wa Kilutheri na hivyo kuweka sharti kuwa vinywaji vinatakiwa viwe ni vile ambavyo havina kilevi.

[17] Spear (1997:135).

[18] Sherehe hizi sasa hivi zimerudia tena kuwa maarufu kutokana na mzozo wa kidini wa hivi karibuni katika Kanisa la Kilutheri (Baroin 1996).

HITIMISHO

Kwa ujumla pombe ya asili ya mbege imepoteza umuhimu wake wa kuwa kinywaji cha kijamii katika jamii ya Wameru ambacho kinatolewa wakati wa posa au mahari au wakati wa ombi lingine lolote na pia kama kinywaji kinachowaleta wazee pamoja kujadili masuala yao ya kifamilia, kijamii au ya kisiasa. Umuhimu wa pombe katika jamii hii umepungua sana na idadi kubwa ya Wameru wameacha kunywa pombe japo bado kuna wanywaji wachache wa pombe hiyo. Bado kuna idadi kadhaa ya ya wanywaji wa pombe, hususan wakati wa jioni, ambao hukutana katika vilabu vya pombe ya mbege ambapo pombe hii bado inatengenezwa na kuuzwa kwa wingi kila siku kama ilivyo kwa Wachaga.[19] Wateja wa sasa huwa ni watu waliozoeleka kuwa wanywaji na wengi ni wanaume japo pia kuna wanawake wachache. Licha ya kuwa pombe ya mbege inauzwa bei nafuu, wanywaji wake hutumia kiasi kikubwa cha fedha katika unywaji huu. Pombe hii huwekwa katika vikombe vikubwa vya plastiki, na ulevi wa wanywaji hususan muda wa jioni sana huweza kusababisha mabishano katika vilabu hivyo. Wateja wa vilabu hivi vya pombe hawafanani kabisa na wale wa kundi lingine la watu wenye kipato kikubwa zaidi ambao huenda katika baa wanakouza bia za chupa ambazo huwa ni ghali zaidi kuliko mbege.

Unywaji wa aina nyingine za pombe hasa bia na konyagi nao umeenea sana siku hizi hasa kwa vijana na watu wenye kipato cha juu. Wazee hupinga vikali unywaji huo wa vijana ambao lengo lake kubwa ni kulewa tofauti na kipindi cha nyuma ambapo watu wazima pekee ndio walikuwa wakinywa pombe kwa lengo la kuburudika na kubadilishana mawazo na siyo kwa kusudi la kulewa. Ulevi wa sasa unatokana na vilevi vipya ambavyo hutokana na molasisi, gongo au ‘pure’ (jina ambalo limetolewa kwenye lugha ya Kiingereza) na pia dadii, pombe ya asili kwa jamii za Wamaasai na Waarusha na ambayo hutengenezwa kwa kutumia nafaka ya mahindi.

Pamoja na kupinga ulevi huo kwa vijana, wazee wanapinga pia kile wanachokiona kama kupotea kwa maadili kiujumla: ukosefu wa heshima kwa wakubwa, kuongezeka kwa uhalifu, pamoja na kushuka kwa maadili ya staha na uvaaji ambako kunaonekana zaidi kwa wasichana. Baadhi ya mabinti wa sasa hupata watoto kabla ya ndoa jambo ambalo halikuwa sahihi katika kizazi cha zamani. Kwa ujumla mabadiliko mengi ya kisasa hayapokelewi vizuri na mathalani, ujauzito kabla ya ndoa unachukuliwa vibaya sana na hata Kanisa nalo pia haliachi kupinga vita tabia hiyo. Hata hivyo tabia ya baadhi ya wanawake vijana kuamua kujihusisha na ukahaba hasa maeneo ya mijini ni ili kujipatia kipato kwa ugumu wa maisha au baada ya kutengwa na familia zao. Hata hivyo Kanisa nalo limeamua kuwatetea kwa njia ya kuwashawishi wazazi kuacha kuwafukuza wasichana mara baada ya kupata mimba nje kabla ya ndoa na badala kuhimiza familia kuwasaidia kuokoa roho za watoto waliowazaa na kuwatunza.

Kubadilika kwa maana na lengo la unywaji wa pombe ndilo jambo ambalo Kanisa pamoja na sehemu kubwa ya jamii vinaliona kama chanzo cha upotevu wa maadili na mmoromoko wa tabia njema. Hali hii ni matokeo ya mageuzi ya haraka mno ya tabia na muundo wa jamii, mageuzi ambayo jamii haijaweza kuendana nayo

[19] Moore (1986:351).

sambamba. Hali kadhalika katika familia nyingi hali hii ya mabadiliko ya kisasa na mmomonyoko wa maadili inahusishwa na kukosekana kwa mipango imara ya kiuchumi kutokana na kuongezeka kwa kasi kwa idadi ya watu na kusababisha uhaba wa ardhi katika eneo la Mlima Meru. Wakati huo huo hakuna mafunzo imara na ya kutosha ambayo yangewezesha vijana kupata ajira mpya au kujiajiri wenyewe. Hiyo ndiyo hali inayoleta mkanganyiko ambao ndani yake unachochea suala la unywaji wa pombe kwa baadhi ya watu wakiwemo hata wale walioingia Ukristo na hivo kuleta utata kwa watu wengi katika jamii hii.

VITABU VYA REJEA

BAROIN, Catherine, 1996, Religious conflict in 1990-1993 among the Rwa: secession in a Lutheran diocese in Northern Tanzania, *African Affairs*, 95, n° 381, uk. 529-554.

BAROIN, Catherine, 1998, Introduction et culture du café chez les Rwa de Tanzanie du Nord, in M. Chastanet (éd.), *Plantes et paysages d'Afrique. Une histoire à explorer.* Paris, Karthala & Orstom, uk. 529-549.

BAROIN, Catherine, 2002, Eleusine et mais, cent ans de cuisine des céréales chez les Rwa (Tanzanie du Nord), in M. Chastanet, D. Jube-Beaulaton et F.-X. Fauvelle-Aymar (éds.), *Cuisine et société en Afrique: histoire, saveurs, savoir-faire*, Paris, Karthala, uk. 265-275.

CORY, Hans, (not dated), Adanyaki Emoti (Breaking the cooking pot), Cory Paper n° 3, 3 typed pages, Dar-es-Salaam.

HARJULA, Raimo, 1969, God and the sun in Meru thought, *Annals of the Finnish society for missiology and ecumenics*, Helsinki, Finland.

HARJULA, Raimo, 1978, Ancestral spirits as helpers among the Meru of Tanzania, *Temenos* (Helsinki, Finland), 14, uk. 53-78.

HARJULA, Raimo, 1989, Curse as a manifestation of broken human relationships among the Meru of Tanzania, in A. Jacobson & Widding et D. Westerlund, (eds), *Culture, experience and pluralism. Essays on African ideas of illness and healing*. Uppsala: *Acta Universitatis Upsaliensis, Uppsala Studies in cultural anthropology* 13, uk. 124 -137.

HARJULA, Raimo, 1997, The ideal of the good life, as crystallized by Tanzanian Meru proverbs, *Studia orientalia*, Helsinki, 81.

ILIFFE, John, 1979*, A Modern History of Tanganyika*, Cambridge: Cambridge University Press.

JAPHET, Kirilo & SEATON, Earl, 1967, *The Meru Land Case*, Nairobi, East African publishing house.

JOLLY, Eric, 1995, La bière de mil dans la société dogon, Thèse de doctorat d'ethnologie, Université de Paris X & Nanterre (France), 2 vol.

KAAYA, Baltazar, 1978, The planting of christianity in Meru. Its conflicts and similarities with the traditional culture of the Wameru. Makumira Lutheran Theological College.

MOORE, Sally Falk, 1986, *Social facts and fabrication. Customary law on Kilimanjaro, 1880 - 1980,* Cambridge, Cambridge University Press.

PEATRIK, Anne-Marie (ed), 1995, Ages et générations: ordres et désordres. Des sociétés au rythme du temps, *L'homme*, 134.

PEATRIK, Anne-Marie (ed), 1999, *La vie à pas contés. Génération, âge et société dans les hautes terres du Kenya (Meru Tigania & Igembe),* Nanterre, Société d'ethnologie.

PURRIT, Paul, 1970, The Meru of Tanzania: a study of their social and political organization, Ph.D., University of Illinois at Urbana Champaign (USA).